JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

**WIZARA YA FEDHA**

# MAELEZO YA MHESHIMIWA DKT. MWIGULU LAMECK NCHEMBA MADELU (MB), WAZIRI WA FEDHA AKIWASILISHA KATIKA KAMATI YA BUNGE ZIMA MAPENDEKEZO YA MFUMO NA UKOMO WA BAJETI YA SERIKALI KWA MWAKA 2025/26

**11 MACHI, 2025**

**MAELEZO YA MHESHIMIWA DKT. MWIGULU LAMECK NCHEMBA MADELU (Mb), WAZIRI WA FEDHA AKIWASILISHA KATIKA KAMATI YA BUNGE ZIMA MAPENDEKEZO YA MFUMO NA UKOMO WA BAJETI YA SERIKALI KWA MWAKA 2025/26**

## 1. UTANGULIZI

1. ***Mheshimiwa Mwenyekiti,*** napenda kutumia nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia afya njema na kutuwezesha kukutana siku hii ya leo kwa ajili ya kuwasilisha Mapendekezo ya Mfumo na Ukomo wa Bajeti ya Serikali kwa Mwaka 2025/26 mbele ya Kamati ya Bunge zima.

2. ***Mheshimiwa Mwenyekiti***, awali ya yote, naomba kutoa shukrani zangu za dhati kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, **Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan** kwa kuendelea kuniamini kuongoza Wizara ya Fedha. Kipekee, napenda kumpongeza kwa dhati Jemedari mpambanaji na mwenye busara, hekima na upendo wa dhati kwa nchi na wananchi wake **Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania** kwa kusimamia utekelezaji wa mpango na bajeti ya Serikali iliyowezesha uboreshaji wa: miundombinu ya kiuchumi ikiwemo barabara, reli, nishati na viwanja vya ndege; huduma za jamii ikiwemo elimu, afya na maji; kuboresha mazingira ya uwekezaji na biashara pamoja na kuimarisha diplomasia. Jitihada hizo za **MAMA** zimewezesha pamoja na mambo mengine: kuongeza wastani wa kipato kwa mwananchi mmoja mmoja; kuongezeka kwa udahili wa wanafunzi katika elimu ya msingi, sekondari, elimu ya kati na juu; upatikanaji wa maji safi na salama mijini na vijijini; upatikanaji wa umeme wa uhakika; na kupungua kwa vifo vya wajawazito na watoto.

3. ***Mheshimiwa Mwenyekiti***, napenda kumpongeza **Mhe. Dkt. Philip Isdor Mpango**, **Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania**, kwa weledi wake katika kumsaidia na kumshauri Mhe. Rais kuongoza Taifa letu. Kadhalika, nampongeza **Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa Mbunge wa jimbo la Ruangwa - Lindi, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania** na Kiongozi wa shughuli za Serikali bungeni, kwa uongozi wake mahiri na kumsaidia Mhe. Rais kufuatilia utekelezaji wa mpango na bajeti ya Serikali. Nitumie fursa hii pia kumpongeza **Mhe. Dkt. Dotto Mashaka Biteko, Mbunge wa jimbo la Bukombe - Geita, Naibu Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Waziri wa Nishati** kwa kuendelea kumsaidia Mhe. Waziri Mkuu katika utekelezaji wa majukumu yake.

4. ***Mheshimiwa Mwenyekiti***, ningependa pia kukupongeza wewe binafsi, pamoja na Naibu Spika kwa kuendelea kuliongoza Bunge letu kwa umahiri na kwa kuzingatia sheria na kanuni zinazoliongoza Bunge hili. Aidha, napenda kuishukuru Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti chini ya **Mwenyekiti** wake **Mhe. Oran Manase Njeza, Mbunge wa Mbeya Vijijini** na **Makamu Mwenyekiti Mhe. Twaha Ally Mpembenwe, Mbunge wa Kibiti** kwa maoni na ushauri wakati wa maandalizi na utekelezaji wa bajeti ya Serikali. Vilevile, ninawapongeza waheshimiwa wabunge wote kwa kuendelea kutekeleza ipasavyo wajibu wao wa kikatiba wa kutunga sheria pamoja na kuishauri na kuisimamia Serikali.

5. ***Mheshimiwa Mwenyekiti***, napenda kumshukuru Naibu Waziri wa Fedha, Mhe. Hamad H. Chande (Mb), Katibu Mkuu Dr. Natu El-Maamry Mwamba, Naibu Makatibu Wakuu, viongozi wa taasisi zilizo chini ya Wizara ya Fedha pamoja na watumishi wote wa Wizara ya Fedha kwa kazi nzuri ya usimamizi wa masuala ya uchumi na fedha pamoja na ushirikiano mzuri wanaoendelea kunipa katika kutekeleza majukumu yangu ya kila siku ya shughuli za Serikali.

6. ***Mheshimiwa Mwenyekiti***, ninawasilisha taarifa hii kwa mujibu wa Kanuni ya 116 (1) na (2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Toleo la Mwaka 2023. Aidha, taarifa hii imegawanyika katika sehemu nne: Sehemu ya Kwanza ni Utangulizi; Sehemu ya Pili ni Mapitio ya Utekelezaji wa Bajeti ya Mwaka 2024/25; Sehemu ya Tatu ni Mapendekezo ya Mfumo na Ukomo wa Bajeti kwa Mwaka 2025/26; na Sehemu ya Nne ni Hitimisho.

## 2. MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA BAJETI YA SERIKALI YA MWAKA 2024/25

7. ***Mheshimiwa Mwenyekiti***, katika bajeti ya mwaka 2024/25, Serikali ililenga kufikia malengo na shabaha za uchumi na bajeti ambapo utekelezaji wake umeonesha mafanikio kutokana na utekelezaji madhubuti wa sera, mikakati na mipango mbalimbali inayotekelezwa na Serikali chini ya uongozi mahiri wa Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Utekelezaji wa baadhi ya malengo hayo ni kama ifuatavyo:

(i) Katika kipindi cha Januari hadi Septemba 2024, Pato halisi la Taifa lilikua kwa wastani wa asilimia 5.6 ikilinganishwa na lengo la ukuaji wa Pato halisi la Taifa la asilimia 5.4 mwaka 2024.

(ii) Katika kipindi cha Julai 2024 hadi Januari 2025, wastani wa mfumuko wa bei umepungua na kufikia asilimia 3.1 ikilinganishwa na lengo la kati ya asilimia 3.0 hadi 5.0.

(iii) Hadi Desemba 2024, akiba ya fedha za kigeni ilikuwa dola za Marekani milioni 5,500.5. Kiasi hicho kilitosheleza uagizaji wa bidhaa na huduma nje ya nchi kwa kipindi kisichopungua miezi 4.5 ikilinganishwa na lengo la miezi 4.0.

8. ***Mheshimiwa Mwenyekiti***, bajeti ya Serikali iliyoidhinishwa na Bunge kwa mwaka 2024/25 ni shilingi bilioni 50,291.4. Katika kipindi cha Julai 2024 hadi Januari 2025, Serikali ilitarajia kukusanya na kutumia jumla ya shilingi bilioni 29,089.9. Katika kipindi hicho, Serikali ilikusanya jumla ya shilingi bilioni 29,305.4, sawa na asilimia 100.7 ya lengo. Ridhaa ya matumizi iliyotolewa katika kipindi hicho ni shilingi bilioni 29,603.8, sawa na asilimia 101.8 ya lengo. Matumizi yalikuwa shilingi bilioni 298.5 zaidi ya mapato yaliyopatikana na yaligharamiwa na mkopo wa muda mfupi kutoka Benki Kuu ambao ni utaratibu wa kawaida kupitia Sheria ya Benki Kuu ya Tanzania, Sura ya 197 inayotoa fursa kwa Serikali kupata mkopo wa muda mfupi kuziba nakisi ya bajeti wakati ikisubiri mapato kutoka vyanzo vilivyoidhinishwa katika bajeti. Ili kutokiuka matakwa ya sheria tajwa na kupunguza ulazima wa kukopa kupitia utaratibu huu, Serikali itaendelea kuchukua hatua za kuimarisha ukusanyaji wa mapato ya ndani na kudhibiti matumizi yasiyo ya lazima.

## 2.1. Mwenendo wa Mapato

### 2.1.1. Mapato ya Ndani

9. ***Mheshimiwa Mwenyekiti***, katika kipindi cha Julai 2024 hadi Januari 2025, mapato ya ndani yalifikia shilingi bilioni 20,113.2, sawa na asilimia 100.2 ya lengo la kukusanya shilingi bilioni 20,076.6, kiwa ni ukuaji wa asilimia 10.7 ikilinganishwa na kipindi kama hicho mwaka 2023/24. Kati ya mapato hayo: mapato yaliyokusanywa na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) yalikuwa shilingi bilioni 17,449.5, sawa na asilimia 101.5 ya lengo la kukusanya shilingi bilioni 17,185.8; mapato yaliyokusanywa na Wizara, Idara Zinazojitegemea, Wakala na Taasisi za Serikali yalikuwa shilingi bilioni 1,838.2, sawa na asilimia 87.4 ya lengo la kukusanya shilingi bilioni 2,102.9; na mapato ya Mamlaka za Serikali za Mitaa yalifikia shilingi bilioni 825.6, sawa na asilimia 104.8 ya lengo la kukusanya shilingi bilioni 788.0. Aidha, Desemba 2024 TRA ilivunja rekodi kwa kufanikiwa kukusanya mapato ya jumla ya shilingi bilioni 3,247.5. Kiwango hiki ni cha juu kukusanywa na TRA kwa mwezi tangu kuanzishwa kwake. Ufanisi huu mkubwa unatokana na

juhudi za Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika kusimamia utekelezaji wa sheria mbalimbali, uboreshaji wa mazingira ya uwekezaji na biashara pamoja na kuhamasisha jamii kwa ujumla kuhusu umuhimu wa kulipa kodi kwa ajili ya upatikanaji wa huduma za jamii na utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

10. ***Mheshimiwa Mwenyekiti,*** katika kipindi kilichobaki hadi Juni 2025, Serikali itaendelea kuchukua hatua mbalimbali za kuimarisha ukusanyaji wa mapato ikiwemo: Kuendelea kuhamasisha umma kuhusu umuhimu wa kutoa na kudai risiti za malipo za kielektroniki za EFD; kuendelea kufanya maboresho ya mifumo ya ukusanyaji wa mapato ili kutatua changamoto mbalimbali zinazojitokeza katika matumizi ya mifumo na kuifanya kuwa rafiki kwa watumiaji; kuendelea kuboresha Mfumo wa TAUSI ili kuhakikisha mapato yote yanakusanywa kupitia mfumo huo na kudhibiti mianya ya upotevu wa mapato; kuendelea kuhimiza taasisi za Serikali zinazotoa huduma kwa pamoja kutumia *control number* jumuishi katika kufanya malipo ya kodi, tozo au ada; na kuendelea kuboresha mazingira ya uwekezaji na biashara.

### 2.1.2. Misaada na Mikopo

11. ***Mheshimiwa Mwenyekiti***, katika kipindi cha Julai 2024 hadi Januari 2025, jumla ya shilingi bilioni 3,767.4 zimepokelewa kutoka kwa Washirika wa Maendeleo, sawa na asilimia 114.3 ya makadirio ya shilingi bilioni 3,294.8 ya kipindi hicho. Mafanikio haya yametokana na juhudi za **mwanadiplomasia namba moja** Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika kudumisha na kuimarisha mahusiano na Washirika wa Maendeleo.

12. ***Mheshimiwa Mwenyekiti***, katika kuharakisha utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo ikiwemo barabara, reli, nishati, viwanja vya ndege, upatikanaji wa huduma za kijamii, Serikali imekopa shilingi bilioni 1,561.4 kutoka vyanzo vya nje vyenye masharti ya kibiashara, sawa na asilimia 89.3 ya lengo la kukopa shilingi bilioni 1,749.1. Aidha, Serikali imekopa shilingi bilioni 3,863.3 katika soko la ndani, sawa na asilimia 97.3 ya lengo la kukopa shilingi bilioni 3,969.4. Kati ya kiasi kilichokopwa, shilingi bilioni 2,264.7 zilitumika kulipia hatifungani zilizoiva na shilingi bilioni 1,598.6 zilitumika kugharamia miradi mbalimbali ya maendeleo.

### 2.2. Mwenendo wa Matumizi

13. ***Mheshimiwa Mwenyekiti***, katika kutekeleza azma ya upatikanaji wa huduma stahiki kwa wananchi, Serikali imeendelea kutekeleza sera za bajeti kwa kuelekeza

fedha katika maeneo ya vipaumbele yenye kuongeza chachu ya ukuaji wa uchumi na kuongeza ajira. Katika kipindi cha Julai 2024 hadi Januari 2025, jumla ya ridhaa ya matumizi iliyotolewa kupitia Mfuko Mkuu wa Serikali ilikuwa shilingi bilioni 29,603.8, sawa na asilimia 101.8 ya lengo la kipindi hicho.

14. ***Mheshimiwa Mwenyekiti,*** baadhi ya mafanikio yaliyopatikana katika utekelezaji wa bajeti katika kipindi cha Julai 2024 hadi Januari 2025 chini ya uongozi mahiri wa Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni pamoja na:

(i) Kufikia lengo la ukusanyaji wa mapato ya ndani kwa asilimia 100.2, sawa na ukuaji wa asilimia 10.7;

(ii) Kuendelea kuimarisha demokrasia nchini kwa kufanikisha Uchaguzi wa Serikali za Mitaa, maandalizi ya Uchaguzi Mkuu ikiwemo maboresho ya Daftari la Kudumu la Wapiga Kura ambapo kiasi cha shilingi bilioni 420.4 kimetolewa;

(iii) Malipo ya mishahara ya watumishi yenye jumla ya shilingi bilioni 6,469.4 na shilingi bilioni 7,368.6 kwa ajili deni la Serikali ambayo yalilipwa kwa wakati;

(iv) Ujenzi na ukarabati wa barabara kuu, barabara za mikoa na wilaya pamoja na ujenzi na ukarabati wa madaraja na vivuko ambapo shilingi bilioni 1,546.0 zimetolewa;

(v) Kuboresha upatikanaji wa huduma za jamii ikiwemo upatikanaji wa dawa, vifaa, vifaa tiba na vitendanishi shilingi bilioni 464.8, ujenzi na ukarabati wa hospitali za wilaya, vituo vya afya na zahanati shilingi bilioni 39.6, usambazaji wa maji safi na salama shilingi bilioni 513.2, mikopo kwa wanafunzi wa elimu ya kati na elimu ya juu shilingi bilioni 325.2, elimu msingi bila ada na mitihani ya kitaifa shilingi bilioni 572.7, ukamilishaji wa miradi viporo ya mabwalo na mabweni katika shule za msingi na sekondari shilingi bilioni 17.0, pamoja na ujenzi na ukarabati wa shule za msingi na sekondari shilingi bilioni 69.8;

(vi) Kuendelea kukamilisha ujenzi wa shule mpya 26 za sekondari za bweni za wasichana, shule moja kwa kila mkoa Tanzania Bara ambapo hadi Januari 2025, jumla ya wanafunzi 6,810 wamedahiliwa katika shule hizo. Aidha, wanafunzi 3,464 wanatarajiwa kudahiliwa kidato cha tano katika shule hizo mwaka 2025;

(vii) Kufanikisha utekelezaji wa miradi ya kimkakati na kielelezo ikiwemo ujenzi wa SGR ambao umeanza kutoa huduma kwa kipande cha kutoka Dar es Salaam – Morogoro – Dodoma na shilingi bilioni 441.6 zimetolewa, Mradi

wa Kufua Umeme wa Maji wa Julius Nyerere umeanza uzalishaji ambapo mitambo nane (8) yenye uwezo wa kufua Megawat 1,880 kati ya mitambo tisa (9) imekamilika na shilingi bilioni 223.3 zimetolewa, miradi ya usafirishaji na usambazaji wa umeme shilingi bilioni 1,119.5 ambapo Serikali imefanikiwa kusambaza umeme katika vijiji vyote 12,318 Tanzania bara, ujenzi wa daraja la Kigongo - Busisi shilingi bilioni 84.6, uendelezaji wa Mji wa Serikali Mtumba shilingi bilioni 237.4; kuendelea na ujenzi wa bandari ya uvuvi ya Kilwa Masoko ambapo shilingi bilioni 45 zimetolewa na ujenzi umefikia asilimia 79.0; na kuendelea kuboresha Shirika la Ndege la Tanzania ambapo shilingi bilioni 355.0 zimetolewa kwa ajili ya ununuzi wa ndege mbili, Boeing 737-7 BBJ na Dreamliner B787-8;

(viii) Ujenzi na ukarabati wa viwanja vya michezo kwa ajili ya maandalizi ya michuano ya AFCON ya mwaka 2027 shilingi bilioni 144.4 zimetolewa;

(ix) Kuendelea kutoa ruzuku ya mbolea tani 388,619.9 kwa wakulima ambapo shilingi bilioni 131.7 zimetumika;

(x) Kuendelea kulipa malimbikizo ya madai ya watumishi wa umma, watoa huduma na wakandarasi ambapo jumla ya shilingi bilioni 705.2 zimelipwa na hivyo kuendelea kuchachua shughuli za kiuchumi;

(xi) Kuongezeka kwa ufanisi wa uendeshaji wa shughuli za bandari ambao umepunguza mrundikano wa meli na mizigo;

(xii) Ununuzi wa tani 444,440.95 za nafaka na hivyo kufikisha hifadhi ya tani 785,003.02 kwa ajili ya kuimarisha usalama wa chakula nchini. Aidha, usalama wa chakula nchini umefikia asilimia 128;

(xiii) Kuendelea kuimarika kwa hali ya ulinzi, amani na usalama nchini kulikowezesha kuvutia uwekezaji wa nje na wananchi kutekeleza shughuli zao mbalimbali za kijamii na kiuchumi;

(xiv) Kuendelea kutoa elimu na msaada wa kisheria kupitia Kampeni ya Msaada wa Kisheria ya MAMA *Samia* ambapo wananchi 1,386,656 kutoka katika halmashauri 120, kata 1,223 na vijiji/mitaa 3,670 wamenufaika. Aidha, madawati ya msaada wa kisheria yameanzishwa katika Mamlaka za Serikali za Mitaa 184. Jumla ya shilingi bilioni 4.95 zimetumika;

(xv) Kuendelea kutekeleza Mkakati wa Taifa wa Matumizi ya Nishati Safi ya Kupikia mwaka 2024 – 2034 kwa lengo la kuboresha afya za wananchi na kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi; na

(xvi) Kuongezeka kwa idadi ya watalii nchini ambapo watalii 1,392,481 waliwasili nchini katika kipindi cha Julai 2024 hadi Januari 2025, sawa na ongezeko la asilimia 13.4 kutoka watalii 1,227,454 katika kipindi kama hicho mwaka 2023/24.

15. ***Mheshimiwa Mwenyekiti,*** katika kuboresha hali ya watu wenye mahitaji maalumu na vijana, Serikali ya awamu ya sita chini ya Jemedari Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ilizindua na kuanza utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Vijana (2007), Toleo la Mwaka 2024 pamoja na Mpango Kazi wa Taifa wa Haki na Ustawi kwa Watu wenye Ualbino 2024/2025 – 2028/2029 (MTHUWWU). Lengo ni kuendeleza na kuboresha hali ya maisha ya vijana na watu wenye ualbino nchini. Aidha, Serikali ilizindua na kuanza utekelezaji wa Mkakati wa Kitaifa wa Teknolojia Saidizi 2024 – 2027 (National Assistive Technology Strategy – NATS) ili kuweka mazingira wezeshi kwa kila mtanzania mwenye uhitaji wa vifaa saidizi kwa gharama nafuu. **HAKIKA KWA MAFANIKIO HAYA MWAKA 2025 WATANZANIA WOTE WATAENDA NA MAMA.**

## 3. MAPENDEKEZO YA MFUMO NA UKOMO WA BAJETI KWA MWAKA 2025/26

### 3.1. Malengo na Misingi ya Uchumi Jumla

16. ***Mheshimiwa Mwenyekiti***, shabaha za uchumi jumla kwa mwaka 2025/26 ni:

(i) Kuongeza kasi ya ukuaji wa uchumi kufikia asilimia 6.0 mwaka 2025 kutoka matarajio ya asilimia 5.4 mwaka 2024;
(ii) Mfumuko wa bei kuendelea kuwa tulivu katika wigo wa tarakimu moja ya wastani wa asilimia kati ya 3.0 - 5.0;
(iii) Mapato ya ndani kufikia asilimia 16.4 ya Pato la Taifa mwaka 2025/26 ikilinganishwa na matarajio ya asilimia 15.8 mwaka 2024/25;
(iv) Mapato ya kodi kufikia asilimia 13.1 ya Pato la Taifa mwaka 2025/26 kutoka matarajio ya asilimia 12.8 mwaka 2024/25;
(v) Nakisi ya bajeti kuwa asilimia 3.5 ya Pato la Taifa mwaka 2025/26 kutoka matarajio ya asilimia 3.4 mwaka 2024/25; na
(vi) Kuwa na akiba ya fedha za kigeni inayokidhi mahitaji ya uagizaji wa bidhaa na huduma kwa kipindi kisichopungua miezi minne (4).

17. ***Mheshimiwa Mwenyekiti***, mapendekezo ya mfumo na ukomo wa bajeti ya Serikali kwa mwaka 2025/26 yameandaliwa kwa kuzingatia misingi ya uchumi jumla ambayo ni:

(i) Kuongezeka kwa ushiriki wa sekta binafsi kwenye shughuli za uchumi;
(ii) Kuendelea kuhimili athari za majanga ya asili na yasiyo ya asili ikiwemo ukame, vita, magonjwa ya mlipuko, mafuriko n.k;

(iii) Kuimarika kwa uchumi wa dunia na utulivu wa bei katika masoko ya fedha na bidhaa;

(iv) Kuendelea kuimarika kwa upatikanaji na usalama wa chakula nchini; na

(v) Kuendelea kuwepo kwa amani, usalama, umoja na utulivu wa ndani na nchi jirani.

### 3.2. Sera za Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2025/26

18. ***Mheshimiwa Mwenyekiti***, mwaka 2025/26, Serikali itaendelea kuweka kipaumbele katika ukusanyaji wa mapato ya ndani kwa kutekeleza mikakati mbalimbali ikiwemo: Kuendelea kusimamia ukusanyaji wa mapato kwa kuimarisha mahusiano mazuri na walipakodi, kuimarisha vyanzo vilivyopo vya mapato pamoja na kutanua wigo kwa kuibua vyanzo vipya; kuunganisha mifumo ya TRA na mifumo ya taasisi nyingine za umma; kuendelea kuhamasisha na kutoa elimu kuhusu matumizi ya mashine za kutolea risiti za kielektroniki; na kuhamasisha matumizi ya malipo ya kidigitali ili kupunguza matumizi ya fedha taslimu.

19. ***Mheshimiwa Mwenyekiti***, mwaka 2025/26, Serikali itaendelea kusimamia utekelezaji wa bajeti kwa kuzingatia Sheria ya Bajeti, Sura ya 439, Sheria ya Fedha za Umma, Sura ya 348, Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa, Sura ya 290 na Sheria ya Ununuzi wa Umma, Sura ya 410. Lengo ni kuhakikisha matumizi sahihi ya fedha za umma na hivyo kuwezesha Serikali kugharamia mahitaji yasiyoepukika hususan mishahara, deni la Serikali na Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2025. Aidha, Serikali itaendelea kuhakiki, kulipa na kuzuia ongezeko la malimbikizo ya madai, kuimarisha matumizi ya mfumo wa ununuzi wa umma (NeST) ili kuendana na ubora na thamani ya fedha, na kuboresha miundombinu wezeshi itakayovutia uwekezaji.

### 3.3. Maeneo ya Kipaumbele kwa Mwaka 2025/26

20. ***Mheshimiwa Mwenyekiti***, bajeti inayopendekezwa inaenda kukamilisha utekelezaji wa Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Miaka Mitano na Dira ya Taifa ya Maendeleo ya 2025. Kwa msingi huo, bajeti imezingatia vipaumbele vya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa mwaka 2025/26 kwa kuendeleza na kukamilisha utekelezaji wa afua zinazochangia maeneo makuu ya vipaumbele vya Mpango ili kuhakikisha ufikiwaji wa malengo ya Dira 2025. Hivyo, vipaumbele vya bajeti ya mwaka 2025/26 vitaendelea kuzingatia maeneo makuu ya Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Miaka Mitano ambayo ni: Kuchochea uchumi shindani na shirikishi; kuimarisha uzalishaji wa bidhaa viwandani na utoaji huduma; kukuza uwekezaji na biashara; na kuchochea maendeleo ya watu na kuendeleza rasilimali watu.

21. ***Mheshimiwa Mwenyekiti***, maeneo mahsusi ya vipaumbele ni pamoja na ugharamiaji wa: deni la Serikali; mishahara; Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2025 na uimarishaji wa demokrasia nchini; kuimarisha amani, utulivu, usalama; na maandalizi ya michuano ya AFCON ya mwaka 2027. Aidha, bajeti hii itahusisha maandalizi ya nyenzo za utekelezaji wa Dira ya Taifa ya Maendeleo ya mwaka 2050. Vilevile, bajeti ya mwaka 2025/26 imezingatia athari zinazoweza kujitokeza kutokana na mabadiliko ya sera za washirika wa maendeleo hususan Marekani.

### 3.4. Mfumo na Ukomo wa Bajeti kwa Mwaka 2025/26

22. ***Mheshimiwa Mwenyekiti***, kwa kuzingatia sera za bajeti na mikakati ya kukusanya mapato pamoja na udhibiti wa matumizi, mfumo na ukomo wa bajeti ya ya Serikali kwa mwaka 2025/26 unapendekezwa kuwa shilingi bilioni 57,040.3, sawa na ongezeko la asilimia 13.4 ikilinganishwa na bajeti ya shilingi bilioni 50,291.4 mwaka 2024/25.

#### 3.4.1. Mapato

23. ***Mheshimiwa Mwenyekiti***, bajeti ya mwaka 2025/26 inatarajiwa kugharamiwa na mapato ya shilingi bilioni 40,966.0 na mikopo ya ndani na nje ya shilingi bilioni 16,074.2. **Mapato** hayo yanajumuisha mapato ya kodi shilingi bilioni 31,826.1, mapato yasiyo ya kodi shilingi bilioni 6,234.5, mapato ya halmashauri shilingi bilioni 1,680.5 na misaada shilingi bilioni 1,224.9. Mapato ya ndani yanatarajia kugharamia asilimia 69.7 ya bajeti yote mwaka 2025/26 ikiwa ni mkakati wa Serikali wa kupunguza utegemezi wa vyanzo visivyotabirika au vyenye masharti na gharama kubwa. Aidha, **mikopo** inajumuisha shilingi bilioni 6,278.2 kutoka vyanzo vya ndani na shilingi bilioni 9,796.1 kutoka vyanzo vya nje.

24. ***Mheshimiwa Mwenyekiti***, ongezeko la makadirio ya mapato limetokana na mikakati mbalimbali ya kiutawala na kisera inayoendelea kuchukuliwa na Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi katika kusimamia ukusanyaji wa mapato kama ilivyoainishwa kwenye Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi ya Mwaka 2020. Hivyo, Serikali itaendelea kutekeleza sera na mikakati ya kuongeza mapato kwa mwaka 2025/26 ikiwemo:

(i) Kuendelea kusimamia ukusanyaji wa mapato kwa kuimarisha vyanzo vilivyopo pamoja na kutanua wigo kwa kuibua vyanzo vipya na kuweka mbinu za kurahisisha utambuzi, usajili, ukadiriaji na ulipaji wa kodi, ada na tozo za Serikali;

(ii) Kuunganisha mifumo ya TRA na mifumo ya taasisi nyingine za umma ili kupata taarifa zitakazowaibua walipakodi ambao hawajasajiliwa ili kuwaingiza kwenye mfumo rasmi wa kodi;

(iii) Kuendelea kuhamasisha na kutoa elimu kuhusu matumizi ya mashine za kutolea risiti za kielektroniki - EFD kupitia uendeshaji wa programu mbalimbali za hamasa ikiwemo tuzo ya uzalendo;

(iv) Kuhakikisha taasisi zenye mlengo wa utoaji huduma kwa pamoja zinaboresha mifumo ya ukusanyaji kwa kutoa namba ya malipo jumuishi ili kurahisisha ulipaji wa kodi, ada na tozo kwa wateja na hivyo kuongeza uhiari wa ulipaji wa kodi;

(v) Kuendelea kuwekeza kwenye matumizi ya teknolojia na kuboresha ushirikiano wa pamoja kwa taasisi za Serikali zinazokusanya mapato kwa lengo la kubadilishana taarifa na mbinu za ukusanyaji ili kupunguza gharama na kuongeza ufanisi;

(vi) Kukabiliana na vitendo vya ukwepaji kodi kwa kuimarisha usimamiaji wa sheria, upatikanaji wa taarifa na kuendelea kujenga uwezo wa watumishi wa umma, hususan kwenye maeneo ya ukaguzi, na uchunguzi;

(vii) Kuendelea kurasimisha sekta isiyo rasmi kwa kuwatambua wazalishaji na wafanyabiashara wadogo wadogo; na

(viii) Kuhamasisha na kuhimiza matumizi ya malipo ya kidigitali ili kupunguza matumizi ya fedha taslimu.

### 3.4.2. Matumizi

25. ***Mheshimiwa Mwenyekiti***, matumizi ya Serikali yanakadiriwa kuwa shilingi bilioni 57,040.3 mwaka 2025/26. Kati ya kiasi hicho, stahiki za watumishi na michango ya pensheni (Serikali Kuu) ni shilingi bilioni 7,711.9, ununuzi wa bidhaa na huduma shilingi bilioni 7,812.2 na fedha zinazoelekezwa kwa baadhi ya taasisi za Serikali, mashirika ya umma na Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa ajili ya matumizi yao (subvention) ni shilingi bilioni 21,407.9. Aidha, ununuzi wa mali ikiwemo vifaa vya ofisi, mashine, magari, samani, ujenzi wa majengo na miundombinu ni shilingi bilioni 3,030.2. Vilevile, Serikali inatarajia kutumia shilingi bilioni 7,715.3 kugharamia malipo ya mtaji na shilingi bilioni 6,493.7 malipo ya riba kwa deni la ndani na nje.

26. ***Mheshimiwa Mwenyekiti,*** kwa kuzingatia Mwongozo wa Kimataifa wa Kuandaa na Kuwasilisha Takwimu za Fedha za Serikali (Government Finance Statistics (GFS) Manual 2014), mchanganuo wa mapendekezo ya mfumo wa bajeti kwa mwaka 2025/26 ni kama unavyoonekana katika **Jedwali Na. 1**.

## Jedwali Na. 1: Mapendekezo ya Mfumo wa Bajeti ya Serikali kwa Mwaka 2025/26

(shilingi milioni)

| | 2024/25 | 2025/26 |
|---|---|---|
| | Bajeti iliyoidhinishwa | Bajeti inayopendekezwa |
| **Mapato** | **35,405,037** | **40,966,016** |
| **Mapato ya kodi** | **28,046,646** | **31,826,123** |
| Kodi za mapato | 9,814,968 | 11,381,400 |
| o/w Kodi ya Ajira (P.A.Y.E) | 5,291,801 | 6,211,331 |
| Kodi itokanayo na orodha ya malipo ya mishahara (Skills Develeopment Levy) | 413,815 | 437,366 |
| Kodi ya majengo/mali | 180,504 | 264,897 |
| Kodi za bidhaa na huduma | 12,115,008 | 13,270,647 |
| o/w Kodi ya Ongezeko la Thamani | 8,234,444 | 9,072,078 |
| Ushuru wa bidhaa | 3,715,879 | 4,113,904 |
| Kodi za biashara za kimataifa | 5,506,649 | 6,428,209 |
| Kodi nyingine | 15,702 | 43,604 |
| **Misaada/Michango** | **794,391** | **1,224,884** |
| Kutoka kwa nchi wahisani | 269,070 | 315,712 |
| Kutoka kwa mashirika ya kimataifa | 525,321 | 909,172 |
| **Mapato mengine** | **6,564,001** | **7,915,009** |
| o/w Mamlaka za Serikali za Mitaa | 1,356,341 | 1,680,507 |
| | | |
| **Matumizi** | **40,367,127** | **46,294,829** |
| **Mishahara na stahiki za watumishi** | **7,498,211** | **7,711,867** |
| o/w Mishahara kwa watumishi wa Serikali Kuu | 4,255,808 | 4,754,850 |
| Michango ya hifadhi za jamii | 1,994,754 | 2,240,141 |
| **Gharama za bidhaa na huduma** | **5,581,970** | **7,812,245** |
| o/w Malipo ya madeni ya watumishi, wazabuni na wakandarasi | 600,000 | 800,000 |
| **Malipo ya riba** | **5,581,973** | **6,493,715** |
| Malipo ya riba nje | 2,435,305 | 2,796,427 |
| Malipo ya riba ndani kwa taasisi zisizo Serikali Kuu | 3,146,668 | 3,697,288 |
| Malipo kwa taasisi ambazo ni Serikali Kuu | - | - |
| **Fedha kutoka Serikali Kuu kwenye taasisi za uwekezaji** | **1,707,591** | **1,936,023** |
| Kwa mashirikia ya umma | 1,665,351 | 1,889,293 |
| o/w Mishahara ya watumishi | 52,397 | 36,718 |
| Kwa sekta nyingine | 42,240 | 46,730 |
| o/w Mishahara ya watumishi | 39,419 | 36,072 |
| **Fedha kutoka Serikali Kuu** | **19,267,768** | **21,407,935** |
| Kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa | 8,830,397 | 9,903,349 |
| o/w Mishahara ya watumishi | 5,361,264 | 6,162,616 |
| Ununuzi wa samani na uwekezaji | 1,447,769 | 1,656,877 |
| Kwa taasisi za umma | 10,323,803 | 11,504,586 |
| o/w Mishahara ya watumishi | 2,059,099 | 2,183,984 |
| Ununuzi wa samani na uwekezaji | 5,307,225 | 6,819,691 |
| **Mafao na misaada ya kijamii** | **623,088** | **752,516** |
| Mafao ya hifadhi za jamii | - | - |
| Misaada ya huduma za jamii | 13,593 | 10,473 |
| Mafao na viinua mgongo | 609,495 | 742,042 |
| **Gharama nyingine** | **106,526** | **180,528** |
| | | |
| **Salio la Mapato na Matumizi** | **(4,962,089)** | **(5,328,813)** |
| | | |
| **Uwekezaji katika mali zisizo za kifedha** | **2,384,789** | **3,030,160** |
| Gharama za majengo, miundombinu, magari, mashine n.k | 2,302,347 | 2,916,037 |
| Mali zisizozalishwa/mali za asili | 82,442 | 114,123 |
| | | |
| **Nakisi ya Bajeti bila Misaada** | **(8,141,269)** | **(9,583,858)** |
| | | |
| **Nakisi ya bajeti ikijumuisha misaada** | **(7,346,878)** | **(8,358,973)** |
| | | |
| **Ugharamiaji wa nakisi ya bajeti** | (7,346,878) | (8,358,973) |
| **Mikopo halisi** | **7,346,878** | **8,358,973** |
| **Mikopo ya ndani** | **2,595,417** | **2,952,630** |
| Mikopo ya ndani | 6,617,790 | 6,278,186 |
| Malipo ya mikopo ya ndani | (4,022,373) | (3,325,557) |
| **Mikopo ya nje** | **4,751,461** | **5,406,343** |
| Mikopo ya nje | 8,268,581 | 9,796,050 |
| Malipo ya mikopo ya nje | (3,517,120) | (4,389,707) |
| | | |
| **Jumla ya Bajeti** | **50,291,408** | **57,040,252** |
| **Nakisi ya bajeti/Pato la Taifa** | 3.4% | 3.5% |

**Chanzo**: Wizara ya Fedha

## 4. HITIMISHO

27. ***Mheshimiwa Mwenyekiti***, mapendekezo ya Mfumo na Ukomo wa Bajeti ya Mwaka 2025/26 yatakuwa ni ya mwisho katika utekelezaji wa Dira ya Taifa ya Maendeleo ya Mwaka 2025 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2021/22 - 2025/26) wenye dhima ya "*Kujenga Uchumi Shindani na Viwanda kwa Maendeleo ya Watu*".

28. ***Mheshimiwa Mwenyekiti***, mwaka 2025/26, Serikali inatarajia kutekeleza mikakati mbalimbali ili kuongeza wigo wa kodi na hivyo kuongeza ukusanyaji wa mapato na kupunguza utegemezi wa kibajeti. Aidha, Serikali itaendelea kusimamia na kudhibiti matumizi kwa kuyawianisha na hali halisi ya upatikanaji wa mapato kwa kutoa kipaumbele kwa mahitaji yasiyoepukika ikiwemo ugharamiaji wa mishahara, deni la Serikali, hati za madai na huduma za jamii. Vilevile, Serikali itaendelea kuweka kipaumbele kwa miradi inayoendelea kwa kuhakikisha inatengewa bajeti katika mwaka 2025/26.

29. ***Mheshimiwa Mwenyekiti***, nichukue fursa hii kuwashauri waheshimiwa wabunge wenzangu kutembea kifua mbele na kunadi mafanikio ya Serikali ya awamu ya sita yaliyoainishwa katika hotuba yangu pamoja na mengine yaliyopatikana chini ya uongozi hodari wa Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi. Mafanikio haya, ni nguzo muhimu kwa wananchi kufanya maamuzi sahihi katika Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2025. Hivyo, nina imani Chama Cha Mapinduzi kitapata tena ridhaa ya kuendelea kuwatumikia watanzania kwa kupata majimbo yote ya uchaguzi. **NANI KAMA MAMA!**

30. ***Mheshimiwa Mwenyekiti,*** naomba kuwasilisha.

Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba Madelu (Mb.),
**WAZIRI WA FEDHA**
11 Machi, 2025